

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2322624
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imepanga kufanya mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau (**Public Hearing**) kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa Mwaka 2019 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.3) Bill, 2019)**, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Muswada huu umesomwa mara ya Kwanza Bungeni tarehe 19 Juni, 2019.

Mkutano huo wa kupokea kusikiliza na maoni ya wadau (**Public Hearing**) utafanyika **siku ya Ijumaa tarehe 21 Juni, 2019 saa 7:00 mchana** na **siku ya Jumamosi tarehe 22 Juni, 2019 saa 4:00 asubuhi** katika ukumbi Na. 9 Jengo la Utawala, Bungeni Jijini Dodoma.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Muswada huu, Kamati inawaalika wadau wote kufika na kuwasilisha maoni yao kabla Muswada huo haujapelekwa katika hatua nyingine. Maoni ya wadau pia yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya posta au Barua pepe kwa anuani ifuatayo:-

Katibu wa Bunge,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

Barua pepe: cna@bunge.go.tz

Muswada huo pia unaweza kupakuliwa kupitia tovuti ya Bunge, www.parliament.go.tz

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

19 Juni, 2019.